MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE
SCHOOL JOINING INSTRUCTIONS

PONGWE ISLAMIC GIRLS SECONDARY SCHOOL

P.O. BOX 907 TANGA



(C) TAMPROS

In the Name of Allah Most Gracious Most Merciful
PONGWE ISLAMIC GIRLS SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 907 Tanga, Mobile +255 715 577 115, 0712 048 197. E-mail: pongweislamic@gmail.com

30/09/2024

Kumb Na. PIGSS/ADM/VOL.1/2024

Ndugu
……..
……..

Assalam Alaykum,

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO I MWAKA 2025

Uongozi wa shule unakupongeza na kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na Kidato I katika shule ya Kiislamu ya wasichana Pongwe mwaka wa masomo 2024.

Soma kwa makini **maagizo** na **kanuni za shule**, baada ya kuzielewa na kukubaliana nazo thibitisha kukubali kwako kwa kujaza fomu ya utambulisho na uthibitisho wa mwanafunzi na wazazi/walezi ambayo imeambatanishwa kwenye barua hii (**Kiambatanisho A**)

Wanafunzi wote wanatakiwa kuripoti shuleni siku ya Jumapili tarehe 01/01/2025 kuanzia saa 07:30 Adhuhuri hadi 12:00 Jioni. Kila **mwanafunzi ni sharti aletwe shuleni na mzazi au mlezi wake** si zaidi ya muda ulioelekezwa ili aweze kupokelewa.

Ulipaji wa ada na michango umeainishwa katika maelezo, ambapo italipwa kwa awamu tatu au moja. ***Mwanafunzi lazima awasilishe malipo kamili ya Ada ya Awamu ya kwanza, michango na vifaa vyote vinavyohitajika ndipo apokelewe.***

Sare za shule na nguo za kushindia zitashonwa shuleni ili kuepusha kuwa na mchanganyiko wa rangi.

Tunakukaribisha *Pongwe Islamic Girls Secondary School*, tunakutakia kila la kheri katika kuishi kwako hapa shuleni.

Wabillah Tawfiiq.

……
MKUU WA SHULE

1. SHULE YA WASICHANA YA KIISLAMU YA PONGWE

Ni shule ya bweni kwa wasichana pekee, kidato I - IV. Shule ipo Tanga mjini - umbali wa kilometa mbili (2) toka Pongwe karibu na shule ya Msingi Maranzara.
Unaweza kufika shuleni kwa usafiri wa pikipiki kwa gharama ya shilingi (1500/=) kutokea Kituo cha basi Pongwe, Barabara kuu ya Tanga-Segera.

Mbali na kutoa elimu ya sekondari, shule imedhamiria;

(i) Kuwawezesha mabinti wa Kiislamu kuitambua hadhi na Jukumu lao katika jamii.
(ii) Kuwaelimisha na kuwalea mabinti, ili kupata viongozi bora wa baadae katika ngazi ya familia na Taifa kwa ujumla.
(iii) Kujenga msingi wa wataalamu wa kike katika fani za sayansi ikiwemo utabibu

2. MASOMO YANAYOFUNDISHWA

Shule inafundisha kwa Mtaala wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi nchini Tanzania. Masomo yanayofundishwa ni, ***Maarifa ya Uislamu, Mathematics, English Language, Arabic Language, Physics, Chemistry, Biology, Geography, History na Civics.***

Masomo 9 ya mtaala hufundishwa kwa njia ya mtandao (TEHAMA) kila mwanafunzi akiwa na tablet (**Kishikwambi**) yake.

Shule inafundisha elimu ya Dini ya Kiislamu kwa mfumo wa Madrassa ikiwemo *Qur'an (Hifdh na Tilawat)*, *Hadith*, *Tawheed*, *Fiqh na Sirat* kwa Lugha ya Kiarabu.

Kila mwanafunzi ni LAZIMA asome Qur'an, Lugha ya Kiarabu na Maarifa ya Uislamu kwa miaka yote minne hata kama hatafanya mtihani wa Taifa.

3. SARE YA SHULE

Sare za shule zinashonwa shuleni, **mwanafunzi haruhusiwi kushona sare nyumbani**. Gharama zimeainishwa katika jedwali ukurasa wa tano (5) wa maelekezo haya.

SARE ZINAZOHITAJIKA	RANGI YA VAZI
a) SARE YA DARASANI	
Suruali (Panjabi) mbili (2)	Darkish Blue
Ushungi mkubwa wa mviringo wa chini ya goti.	Nyeupe
Nusu kanzu mbili (2) chini ya goti na mikono mirefu	Darkish Blue
Baibui moja (1) itakayovaliwa juu baada ya suruali na nusu kanzu	Darkish Blue
Viatu vya kufunika mguu visivyo na kisigino kirefu vyenye kamba (Kisigino wastani wa nchi 1) (**Aje navyo**)	Vyeusi
Soksi jozi mbili (2) (**Aje nazo**)	Nyeupe
b) SARE YA NJE YA DARASA	
Baibui refu lisilopasuliwa mbele.	Blue Masai
Ushungi mkubwa wa mviringo urefu chini ya goti.	Blue Masai
Jozi (1) Kanga na Kitenge, Baibui jeusi na shungi lake. (**Aje nazo**)	Nyeusi
Simple Raba (**Aje nazo**) haturuhusu open shoes zaidi ya ndala za kuogea	Maruni
Aje na baibui na shungi kuvaa akisubiri sare za shule	Nyeusi

4. VIFAA VYA MASOMO NA BWENINI VINATOLEWA SHULENI

Kila mwanafunzi analazimika kuwa na vifaa vya masomo ambavyo vitatolewa na shule kwa gharama (240,000/=) imeainishwa hapo chini;

a) Godoro 55,000/=
b) Shuka 2 (Blue bahari na pink) = 18,000/=
c) Trunk 25,000/=
d) Daftari 15 (3 Quires 10 @ 3,500 na 4 Quire 5 @ 4,500/=
e) Chandarua 12,000/=
f) Rimu A4 15,000/= na Rimu ya mistari 12,500/=
g) Mkebe 3,500/=
h) Ndoo, beseni, sahani, kikombe na bakuli 15,500/=
i) Graph paper 2 @ 4,000/=
j) Seti ya penseli za rangi 4,000/=
k) Jembe na mpini 14,000/=

5. VIFAA VYA HOSTELI NA USAFI

Vifaa vilivyoorodheshwa hapo chini kila mwanafunzi aje navyo shuleni siku ya kuripoti.

(i) Taulo, malapa na mswaki.
(ii) Chupa ya kuhifadhia maji ya moto.
(iii) Sabuni ya kufulia na kuogea.
(iv) Sweta la kufuma rangi blue (kuvaa wakati wa baridi)
(v) Past it Note dozen 1 na kalamu za kutosha.
(vi) Vifaa vya madrasa (Msahafu chapa ya Saudi na daftari sita (6) za msomi.
(vii) Mkoba wa Madaftari (Begi Jeusi)
(viii) Soft broom 1

NB. *Mwanafunzi atakapoacha, kufukuzwa au kuhama shule vifaa vyake kama vile godoro sanduku n.k anatakiwa kuondoka navyo.*

6. ADA NA MICHANGO YA SHULE

i. Ada kwa mwaka wa masomo 2024 inalipwa kwa awamu tatu kama inavyoainishwa katika jedwali hapo chini.

MAELEZO	AWAMU ZA MALIPO YA ADA		
Malipo Yanafanywa Wiki ya Kwanza ya Mwezi Tajwa	1. Januari	2. April	3. Julai
	800,000/=	650,000/=	400,000/=

ii. Mchango wa Bima ya Afya 75,000/= kulipia bima, na usafiri wa hospitali.

iii. Mchango wa Tablet (Kishikwambi) 270,000/= kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza na wanaohamia kidato cha pili na tatu, ufundishaji na ujifunzaji utatumia teknolojia.

iv. Malipo ya ada na michango yafanyike kupitia akaunti zilizoainishwa katika jedwali hapo chini;

Akaunti za Kulipia Ada		**Jina la Akaunti zote**	**Akaunti ya kulipia Michango**	
CRDB	**Acc Na: 0150705966600**	Pongwe Islamic Girls Sec School	Amana Bank	Acc Na **008121053180001**
DTB	**Acc Na: 0035678001**			

v. Michango ifuatayo iwasilishwe shuleni siku atakaporipoti mwanafunzi;

Aina ya mchango	Kiasi TShs.
Usajili	10,000.00
Ukarabati	10,000.00
Nembo ya shule (1)	5000.00
Kitambulisho	5000.00
Mahafali kidato IV- 2025	15,000.00
Ukaguzi na michezo	10,000.00
Mitihani ya ila wiki	10,000.00
Sare za Shule jozi 2@ 80,000/=	160,000.00
Sare ya Kushindia jozi 2@ 40,000/=	80,000.00
JUMLA KUU	**305,000.00**

7. UANDIKISHWAJI

Siku ya kuripoti shuleni mwanafunzi awe na vifaa vifuatavyo;

(i) Fomu za maelezo ya mzazi / mlezi kuhusu utambulisho wa mwanafunzi na wazazi / walezi (Kiambatanisho A)

(ii) Fomu maelezo yaliyothibitishwa na daktari (*Medical Examination Report*) (Kiambatanisho B).

(iii) Stakabadhi ya Malipo ya Benki (Pay in Slip)

(iv) Picha tatu (3) za passport size au TShs 3000/=.

(v) Uthibitisho wa Kumaliza Darasa la Saba (VII) (**Namba ya PLSE**)

(vi) Nakala ya Cheti cha Kuzaliwa.

8. MAENDELEO YA DARASANI

Ili kufaulu kuingia Kidato II mwanafunzi anatakiwa afikishe wastani wa alama zisizopungua 55% na Credit saba (7) au zaidi kwa mwanafunzi atakaeingia Kidato IV.

Somo la Maarifa ya Uislamu na Lugha ya Kiarabu yanachukua uzito wa pekee hivyo kila mwanafunzi analazimika kufanya bidii na kuhakikisha anafaulu angalau kwa kiwango cha daraja 'B'.

9. KUTEUA MASOMO

(i) Mwanafunzi atakayefaulu kuingia Kidato cha Tatu atachagua masomo katika tahasusi za *Sayansi ya Jamii*, *Lugha*, *Sayansi*, *Sanaa na Dini* kulingana na masomo yanayofundishwa shuleni.

(ii) Uchaguzi wa masomo utazingatia uwezo wa mwanafunzi, utashi wake, ushauri wa wazazi/walezi na walimu wa masomo husika atakuwa na nafasi kubwa zaidi katika maamuzi hayo.

10. KUTEMBELEA WANAFUNZI

Shule inatoa fursa kwa wazazi /walezi kutembelea wanafunzi kila **Jumapili ya mwisho** wa mwezi isipokuwa kipindi cha mitihani ama pale ambapo shule itakapoarifu vinginevyo. **Pamoja na ruhusa hiyo mzazi/mlezi haruhusiwi kumletea mwanafunzi chakula cha aina yoyote.**

11. KANUNI NA MWENENDO BORA WA SHULE

(i) Wanafunzi wote wanapaswa kufahamu kuwa chochote kilicho nje ya maadili mema hakina nafasi hapa shuleni.
(ii) Kila mwanafunzi hana budi kujipamba na vipengele vya tabia njema.
(iii) Kila mwanafunzi atawajibika kuzingatia na kufuata kikamilifu ratiba na kalenda ya shule.
(iv) Mwanafunzi atakuwa kajifukuzisha shule mwenyewe iwapo hatafika shule kwa **siku ishirini na moja (21)** bila taarifa zozote shuleni. Taarifa iwe kabla na wala si baada ya tukio la utoro.
(v) Wakati wa masomo wanafunzi wote watabaki shuleni, hawataruhusiwa kutoka ndani ya shule isipokuwa kwa kibali maalum.
(vi) Mwanafunzi atakaekuwa na Wastani wa mahudhurio chini ya asilimia themanini na moja (81%) hatoruhusiwa kufanya mtihani, hivyo hatoruhusiwa pia kuendelea na Kidato kinachofuata, baadala yake atarudia mwaka au kufukuzwa shule.
(vii) Wakati wote wa kuwa shule, **vazi rasmi ni sare ya shule**, **kinyume chake ni kosa**. Mwanafunzi atavaa na kuzingatia maadili hata awapo nje ya shule.
(viii) Mwanafunzi ataripoti tatizo kwanza kwa Head Girl kisha ndipo amwone mwalimu wa zamu, darasa au nidhamu.
(ix) Kelele au zogo hairuhusiwi katika eneo la shule, mazungumzo yote hayanabudi kufuata nidhamu na maadili.
(x) Hairuhusiwi wanafunzi kuja shuleni na chakula cha aina yoyote ama kuletewa zawadi ya chakula na mzazi/mlezi wakati atakapotembelewa.
(xi) Ni marufuku kwa mwanafunzi kujipamba kwa rangi za kucha, nywele, midomo, kupaka wanja, kunyoa nyusi, kuvaa hereni, bangili, mkufu au pete.
(xii) Hairuhusiwi kufanya sherehe za Birtdhday na au Valentine Day kwa namna yoyote shuleni.
(xiii) Hairihusiwi kulala zaidi ya mwanafunzi mmoja katika kitanda kimoja.
(xiv) Vifaa vya electronics kama vile **simu** au **line, mp3, ipod, camera, radio, radio cassette** n.k haviruhusiwi mwanafunzi kuwa navyo katika mazingira ya shule.
(xv) Mbali na kuvunja kanuni hizi halali za shule mwanafunzi atajifukuzisha shule mwenyewe iwapo atajihusisha na ulevi, uesherati na uzinifu.

❖ ***Mamlaka ya shule ndio yenye maamuzi ya mwisho katika kutekeleza kanuni hizi.***

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE

Pamoja na maelezo yote hayo. Mwanafunzi atakayechupa kwa makusudi maadili na kanuni za shule kwa kutenda makosa makubwa kama yalivyoainishwa hapo chini atafukuzwa shule:

a. Kunywa pombe
b. Kwenda nyumba za starehe kama vile kwenye kumbi za madansi, disko n.k
c. Uzinzi, ushoga au kukaribia zinaa kwa namna yeyote.
d. Kuvuta bangi, madawa ya kulevya, n.k
e. Kutosimamisha swala.
f. Kumiliki vitu vya electronics kinyume na maelekezo ya shule ikiwemo **simu au line, mp3, iPad, radio, kamera, kishikwambi kisichokuwa cha shuleni** n.k
g. Kutoroka shuleni
h. Kugomea adhabu stahiki kwa makusudi.
i. Kupata mimba au kutoa mimba ndani na nje ya shule
j. Kuanzisha, kuchochea, kushiriki au kuongoza mgomo.
k. Kuhatarisha amani ya shule kwa kupigana au kuchochea watu wapigane
l. Wizi, uporaji na uharibifu wa mali ya shule na ya wanafunzi au wakazi wa kituo.
m. Kukosa mitihani/jaribio bila ya sababu za msingi.
n. Kutohudhuria masomo/darasani bila sababu maalumu za msingi.

HITIMISHO

Ni matumaini yetu kuwa Mzazi/Mlezi na mwanafunzi mtarajiwa mmeyasoma maelezo haya kwa makini tayari kwa utekelezaji.
Baada ya kujiunga na shule utekelezaji wa kanuni na taratibu za shule kwa mwanafunzi na Mzazi/Mlezi ni wajibu

Mzazi / Mlezi mlete mwanao PONGWE ISLAMIC GIRLS SECONDARY SCHOOL yenye mazingira mazuri ya kimalezi ili aweze kupata masomo na maadili mema kwa maslahi ya mtoto, wazazi, na jamii kwa ujumla.

TUNAKUTAKIA MAISHA MEMA NA KARIBU SANA

……

MKUU WA SHULE



Contact us;

Pongwe Islamic Girls Secondary School

P.O.Box 907, Tanga, TANZANIA.

TEL +255 715577115, +255 713 549 504,
+255 784 577 115

Website: https://www.pongweislamicgirls.ac.tz

E-mail: *info@pongweislamicgirls.ac.tz*

Follow us on *Pongweislamicgirls*